



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA SENGEREMA
MKOA WA MWANZA**



Kumb. Na. AB.16/194/02/VOL.II/02/93

Tarehe: 13/03/2023.

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI KWA MKATABA.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema anapenda kuwatangazia nafasi za kazi kwa Mkataba wa mwaka mmoja (1).

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema anakaribisha maombi ya kazi kutoka kwa watazania wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi wazi za kazi kama ilivyoainishwa katika Tangazo hili:--

1: AFISA AFYA MAZINGIRA MSAIDIZI DARAJA LA II – (NAFASI 5)

1.1: SIFA ZA MWOMBAJI

- Kuajiliwa mwenye Stashahada ya Sayansi ya Afya ya Mazingira kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali na awe amesajiliwa na Bodi ya wataalamu wa Afya Mazingira.

1.2: MAJUKUMU YA AFISA AFYA MAZINGIRA MSAIDIZI DARAJA LA II .

- Kudhibiti na kuzuia milipuko ya magonjwa
- Kupambana na kuzuia wadudu na Wanyama wanaoeneza magonjwa
- Kusimamia uzikaji wa maiti zisizotambuliwa na zile zinazotokana na magonjwa ya kuambukiza.
- Kuandaa taarifa mbalimbali za Afya ya mazingira katika ngazi ya Kata na kuziwasilisha katika mamlaka husika.
- Kukusanya na kuchambua takwimu za Afya ya mazingira, katika Kata na kutoa mrejesho ili kuchukua hatua zinazostahili.
- Kutoa elimu ya Afya ya Mazingira kwa Jamii
- Kukagua mazingira katika sehemu zinapotengenezwa vyakula ili kuhakikisha usalama wa Afya ya Jamii.
- Kusimamia sheria za Afya ya mazingira katika ngazi ya Kata pamoja na kusaidia Jamii katika kutengeneza sharia ndogo ndogo
- Kuhamasisha jamii kuhusu utekelezaji wa Huduma za Afya ya Msingi katika ngazi ya Kata.
- Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na Mkuu wake wa kazi zinazohusiana na Elimu, uzoefu na ujuzi wake.


1.3: MSHAHARA.

Motisha (Special Allowance) kwa kiwango kisichizidi asilimia 50 ya basic salary

MASHARTI KWA UJUMLA.

- i. Mwombaji anatakiwa awe Raia wa Tanzania na mwenye umri usiozidi miaka 45.
- ii. Mwombaji aambatishe cheti cha kuzaliwa
- iii. Mwombaji aambatishe maelezo binafsi yanayojitosheliza (Detailed C.V) yenye anwani na namba za simu zinazopatikana pamoja na majina ya Wadhamini (referees) watatu wa kuaminika.
- iv. Maombi yote yaambatishwe na vyeti vya taaluma, maelezo, nakala za vyeti vya Kidato cha nne na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika.
 - ✓ Certificates
 - ✓ Cheti cha mtihani wa Kidato cha IV.
 - ✓ Vyeti vya kitaaluma (Professional certificate from respective boards)
 - ✓ Picha mbili "Passport size" ya hivi karibuni.
- v. Testmonial", "Provisional Results", "Statement of Results", hati matokeo za kidato cha nne (FORM IV RESULTS SLIPS) HAVITAKUBALIWA
- vi. Mwombaji aliyesoma nje ya Tanzania ahakikishe vyeti vyake vimehakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika (TCU au NECTA).
- vii. Mwombaji wa nafasi ya Ajira aliyestaafishwa/kuachishwa kazi katika Utumishi wa Umma haruhusiwi kuomba isipokuwa kama anakibali cha Katibu Mkuu Kiongozi.
- viii. Mwombaji wa kazi ambaye tayari ni mwajiriwa katika nafasi ya kuingilia aliyeko katika Utumishi wa Umma asiombe kwa kuzingati maelekezo yaliyo katika Waraka Na. CAC. 45/257/01/D/140 wa tarehe 30 Novemba, 2010.
- ix. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kughushi wahusika watachuliwa hatua za sheria.
- x. Mwisho wa kupokea maombi ya kazi ni tarehe 26 Machi, 2023 saa 9.30 Alasiri..
- xi. Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu uliobainishwa katika tangazo hili HAYATAFIKIRIWA.
- xii. Maombi yote yatumwe kwa njia ya Posta kupitia anuani ifuatayo:-

Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema
S.L.P.175,
SENGEREMA.


Binuru M. Shekidele.

MKURUGENZI MTENDAJI (W),

SENGEREMA

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA
S. L. P. 175
SENGEREMA

Nakala: Mbao zote za Matangazo
Halmashauri ya Wilaya,
SENGEREMA.